19. MUNGU AWALINDA WATU WAKE JANGWANI

"Aliwaongoza jangwani kama kundi la Kondoo"

Shabaha

Kuonyesha jinsi Mungu alivyowalinda watu wake jangwani.

Kwa upande mwingine wa bahari ya Shamu wana wa Israeli walikuwa bado wanaongozwa na wingu wakipita katika jangwa la Shuri,mbele yao sasa kulikuwa na umbali wa maili nyingi kupita katika vilima vya mchanga. Kwa siku tatu walivuka katika nchi hii ya upweke bila ya kupata maji mahali popote, na hatimaye wakafika Mara.

Kutoka 15:22 – 27,16;17.

MAJI KATIKA MARA: Kutoka 15:23 – 26 na ELIMU: Kutoka 15:27

Baada ya safari ndefu ya joto kali sana, umati mkubwa wa wana wa Israeli ulifika Mara. Hatimaye hapa palikuwa na maji- lakini walichukizwa sana kuyakuta maji ambayo ni machungu yasiyofaa kwa kunywa, watu wakamnung`ukia Musa: **"tutakunywa nini?"-** kana kwamba Musa angewatafutia maji yanayofaa! Hata hivyo kama ilivyokuwa wakati wa matatizo Musa alimwomba Mungu ili amsaadie.

Mungu alimwambia aweke mti fulani katika maji na maji machungu yatakuwa matamu (mstari 25) Mungu alikuwa hajawaacha,na kila mara aliwapatia mahitaji yao,lakini walikuwa na mafundisho mengi ya kujifunza na Mungu alikuwa akiwapima imani zao.Kama wangesiliza kwa makini maneno yake, ambayo Musa mara nyingi alikuwa akiwaambia na kuzitii amri zake, Mungu asingeweza kuwaletea wao maradhi yoyote ambayo yaliwapata Wamisri.Kama alivyo yatibu maji machungu pale Mara,vivyo hivyo angewalinda kama wangeendelea kumwamini.

Kutoka Mara walisafiri hadi wakafika Elimu-Hapa palikuwa na maji mengi ya kivuli-visima kumi na mbili na tende sabini, na waliweka kambi hapo karibu na maji.(Mstari 27)

MUNGU ANAWAPA CHAKULA WATU WAKE JANGWANI: Kutoka 16:1- 36

Tena wana wa Israeli waliondoka na kuweka kambi kandoni ya bahari ya Shamu (Hes. 33:10). Palikuwa na umbali wa kilometa nyingi kusini ya sehemu walipokuwa wamevukia na bila shaka walikumbuka kuwa ukiyavuka maji utakuwa umekaribia Misri na wasingeweza kurudi nyuma nyuma Misri.Zilikuwa ni juma nne(Mwezi mmoja) tangu siku ya kutoka (kuondoka) katika Misri. Mungu aliwapatia mahitaji yao yote, lakini njia haikuwa rahisi wakalalamika na kunung'unika na wakawagekukia Musa na Haruni wakisema **"Kwani mmetutoa huko na kututia katika bara hii ili kutuua kwa njaa kusanyiko hili lote** (mstari 3);Walikuwa na njaa na walifikiria Misri tu kuwa mahali ambapo **"tulikula vyakula hadi tukashiba"** (mstari 3) walisahau utumwa na ukatili wa mabwana zao wamisri; walisahau kwa nini Mungu aliwatoa kutoka katika Misri na Nchi ya Ahadi pia ilikuwa mbele yao.

Mungu alisikia malalamiko yao na kumwambia Musa **"Tazama mimi nitawanyeshea ninyi mvua ya mikate kutoka mbinguni** (mstari 4).Kisha tena Mungu angetumia uweza nguvu zake na kumaliza manung'uniko yao kwa miujiza ya ajabu.

Wakati wa jioni watakula nyama (mstari 12) na wakati wa asubuhi watakula mikate **"Ikawa wakati wa jioni kware wakakaribia wakakifunikiza kituo,na wakati wa asubuhi umande ulikuwa juu ya nchi pande zote za kituo"** (mstari 13).Baada ya umande kuwa umeyeyuka juu ya ardhi walikuta **"mana"** hiki kilikuwa ni kitu kidogo kilichoviringana nacho kilikuwa mfano wa chembe za mtama nyeupe, na tamu yake ilikuwa kama tamu ya maandazi membamba yaliyoandaliwa kwa asali (mstari 31). Na wao walipokiona walisema **"mana"** ikiwa na maana **"Hiki ni nini?"** (mstari 15). Na hivyo ndivyoo walivyokiita. Huu ndiyo mkate ambao Mungu alikuwa amewaahidi.Na wana wa Israeli walikuwa wamepewa maagizo maalumu jinsi ya kukiokota chakula hiki; kilikiwa kiokotwe kama Mungu alivyokuwa amewaagiza tu.

Waliambiwa kukiokota "**kila siku kila mtu kwa jinsi atakavyo kula"** (mstari 18). Kama walikusanya zaidi ya mahitaji yao kwa siku moja kilioza usiku huo huo na kiliingiza mafunza na kutoa uvundo (mstari 20).

Lakini katika siku ya sita waliweza kuokota chakula cha kutosha siku mbili ili waweze kupumzika siku ya saba ambayo ilikuwa Sabato. Kiliweza kutosheleza kwa siku hizo mbili.

Mana hiyo walipewa wana wa Israeli kila siku kwa muda wa miaka arobaini ambayo walikuwa jangwani(mstari 35).

Mungu hakusahau kamwe kuwapatia chakula.

MUNGU ANAWAPATIA MAJI KUTOKA KATIKA MWAMBA :Kutoka 17:1 – 7

Tena wana wa Israeli walihamisha kambi na wakafika Rephidimu na hapakuwa na maji ya kunywa watu (mstari 1).Wakiwa na woga wa kufa, mara nyingine tena walimng'unikia Musa.

Ilikuwa ni kazi ngumu ya kiasi gani kwa Musa pamoja na mafunzo yote aliyoyapata kuliongoza kundi hili kubwa la watu. Musa alimlilia BWANA **"Niwatendee nini watu hawa bado kitambo kidogo nao watanipiga kwa mawe"** (mstari 4). Mungu akamwambia Musa kuchukua fimbo yake na kwenda na wazee wana wa Israeli kwenye mwamba katika Horebu na kuupiga mwamba kwa fimbo yake. Alipopiga mwamba kwa fimbo, maji yalitiririka kutoka katika mwamba kama mto! Hapa,yakatokea maji mengi kwa umati wa watu waliokuwa na kiu, Mungu alifanya tena muujiza mwingine mbele ya macho yao, wakiwa na Mungu mwenye uwezo wa kuwalinda hawakuwa na sababu gani ya kuwa na wasiwasi wa mahitaji yao ya kila siku.

WAAMALEKI WAWASHAMBULIA WAISRAELI KATIKA REFIDIMU: Kutoka 17:8 – 16

Aina mpya sasa ya hatari ikawatisha wana wa Israeli walipokuwa wakisafiri,vikosi vya Waamaleki ghafla wakawashambulia wakitokea nyuma yao **"Jinsi alivyokukuta katika njia akapiga watu wako walioachwa nyuma wote waliokuwa wanyonge nyuma yako"** (Kumbukumbu Torati 25:18). Hili lilikuwa ni jambo la woga kulifanya.Ilionekana kama wana wa Israeli ambao hawa wamejiandaa wangeshindwa.

Musa alimteua kijana mwaminifu aliyeitwa Yoshua kuwa kamanda na kumwambia **"Tuchagulie watu,utoke na ukapigane na waamaleki"**(mstari 9).Vita vya kutisha,walipigana katika bonde wakati Musa,Haruni na Huri wakiangalia kutoka juu ya mlima. **"Na ikawa Musa alipoinua mkono wake wana wa Israeli walishinda,na alipoushusha mkono wake, Amaleki walishinda"** (mstari11). Kwa hiyo ikiwa kwamba Musa alipounyosha mkono wake juu kwa sala, wana wa Israeli walishinda!Hata ikawa mikono ya Musa ilipochoka na kuwa mizito, Haruni na Huri wakaitegemeza mikono ya Musa kiwa ameketi juu ya jiwe akipumzika, alibakia pale hadi mwisho wa siku mpaka hatimaye wana wa Israeli wakashinda vita vya kutisha dhidi ya jeshi la Amaleki (mistari 11 – 14). Hivyo Mungu alionyesha uwezo wa nguvu zake na ulinzi wake kwa wale wenye kumtegemea yeye. **"Heri taifa ambalo BWANA, ni Mungu wao na watu aliowachagua kuwa urithi wake"** (Zaburi 33:12 – 16)

Vita vikaisha .Watu wakarejea kambini na huko Musa alijenga madhabahu, ilikuwa ni kuwakumbusha wana wa Israeli juu ya vita hii. Mungu alimwambia Musa kuandika habari yote katika kitabu kwa sababu Mungu alidhamiria wana wa Israeli wanakumbuka waamaleki kuwa ni maadui wao milele.Maombi ya Musa yalikuwa na nguvu sana siku ile,na Mungu siku zote anajibu maombi ya wanaume na wanawake waaminifu wakati wa matatizo.

FUNDISHO KWETU

Mungu huwabariki wale ambao wanaweka imani yao kwake.Hii haina maana kwamba Mungu atatupatia chochote tunachotaka, lakini tunajifunza katika somo hili kuwa atatupatia yote tunayohitaji.Aliwapa wana wa Israeli chakula, maji na ulinzi kwa muda wa miaka arobaini wangeomba nini zaidi wakati mbele yao kulikuwa na Nchi ya Ahadi pia!!! Hata nguo zao na viatu vyao havikuchakaa na miguu yao haikuvimba, ingawa walitembea maili nyingi sana. Mwishowe Musa aliwakumbusha juu ya mambo yote haya kabla ya kufa kwake. Watu wengi leo katika dunia wanafariki kwa sababu hawana chakula cha kutosha, mavazi au mahali pa kuishi. Mungu wakati wote anatupatia mahitaji yetu na ametupatia ahadi ya uzima wa milele katika ufalme wake pia.

Kamwe tusinung'unike, lakini kila mara tumshukuru na kumtegemea Mungu anayetupatia mahitaji.

MAELEZO YA NYONGEZA

Mungu hakuyarahisisha mambo kwa wana wa Israeli jangwani. Hii ingekuwa sawa na kuwaharibu.Alitaka wajithibitishe wenyewe kuwa wanastahimili yale yote Mungu aliyoyaweka kwa ajili yao,ili kwamba waweze kuthamini wema wake wote na upendo wake kwao.Musa aliwakumbusha mambo yote haya mapema kabla ya kufa **"Mungu akakuongoza miaka hii arobaini katika jangwa ili akunyenyeze, ili kujuyajua yaliyo moyoni mwako kwamba utashika amri zake au sivyo"** (Kumbukumbu la Torati 8:2). Mungu akawaacha wawe na njaa ili watakapopewa mana waweze kushukuru kwa dhati. Akawaacha wawe na kiu ili kwamba wamshukuru kwa dhati kutokana na miujiza ya kuponywa kwa maji machungu, na maji kutoka ndani ya mwamba. Aliwaruhusu Waamaleki wawashambulie ili waweze kujua kwamba Mungu anatoa ushindi tunapoomba msaada.

Katika yote haya fundisho lilikuwa kwamba **"apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu hataishi kwa mtate tu"** (Kumbukumbu la Torati 8:3) .Bwana Yesu Kristo alipojaribiwa jangwani kwa siku arobaini alinukuu maneno haya kwa yule aliyemjaribu alipokuwa na njaa. Alitumia muda wake wote kujifunza somo hili, mawazo yake yote yalijazwa na neno la Mungu na ndiyo jinsi alivyoshinda dhambi, kwa njia kama hii ni lazima tusome neno la Mungu kila siku na kufikiri juu ya mafunzo yake. **"Yaweza kutuhekimisha hata kupata wokovu"** (2 Timotheo 3:15). Mana hiyo waliyopewa wana wa Israeli kila siku kwa muda wote wa miaka arobaini ambayo walikuwa jangwani (mstari 35) .Tunaweza kujua kuchagua jema na kukata lililo baya.Kwa hiyo tabia yetu itaongeza na kuwa tabia ya Bwana Yesu Kristo,ambaye anaitwa **"mkate wa uzima",** kwa sababu **"yeye anayekuja kwangu hataona njaa kamwe na yeye aniaminiye mimi hataona kiu kamwe"**(Yohana 6:35)

MASWALI

Majibu mafupi

1. Ni jambo gani lililotokea kuhusiana na maji pale Mara?
2. Musa aliambiwa afanye nini ili maji yaweze kufaa kwa kunywa?
3. Ni chakula gani Mungu aliwapatia mkutano mkubwa wa wana wa Israeli walipomnung'unikia karibu na bahari Shamu?
4. Neno **"mana"** lina maana gani?
5. Ni jinsi gani watu walivyopewa maji pale Refidimu?
6. Ni taifa gani baya lililowashambulia wana wa Israeli pale Refidimu?
7. Musa alifanya nini wakati vita vilipokuwa vikiendelea pale Refidimu?
8. Ni nani aliyekuwa kijana mwaminifu aliyeteuliwa na Musa kuongoza wana wa Israeli kupigana na Waamaleki?

Majibu ya Kina

1. Elezjinsi Mungu alivyowapatia mana na maagizo maalumu ambayo Mungu aliwapa ya jinsi ya kuikota?
2. Ni namna gani Mungu alivyowapatia kusanyiko kubwa la wana wa Israeli katika jangwa na tunapata fundisho gani chakula na majikuwashinda waamaleki kule Refidimu na tukanajifunza nini kutokana na somo hili.
3. Fafanua jinsi taifa la Israeli lilivyoweza kupata ushindi dhidi ya Amaleki pale Rephidimu na tunajinza nini kutokana na somo hili?

Majibu ya Nyongeza

4. Ni kwa nini Mungu aliruhusu watu wake wapatwe na njaa na kiu kabla hajawapatia chakula na maji?
5. Ni nani ambaye ndiye mkate wa uzima?
6. Yesu ,kama wana wa Israeli, alikuwa na njaa sana kule jangwani. Ni jinsi gani tabia ya Yesu ilivyotofautiana na ile ya watu wa Israeli?